



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu,
S. L. P 1288 Kishapu, Simu 0282770020, Nukushi 0282770019,
Barua pepe: info@kishapudc.go.tz Tovuti: www.kishapudc.go.tz



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na.KDC.B.20/11/VOL.II/75

16/11/2020

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Kwa mujibu wa kibali cha ajira mbadala chenye Kumb. Na. FA.170/376/01'A'/16 cha tarehe 30/09/2020 kutoka Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu anawatangazia wananchi wote Raia wa Tanzania kuomba nafasi ya Kazi ifuatazo:-

1. Mtendaji wa kijiji Daraja III - (NAFASI -1)

i. Sifa za mwomabaji

- Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha nne au sita
- waliopata mafunzo katika ngazi ya **Cheti** ambao wamejiimarisha katika fani zifuatazo:-

Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya sanaa, kutoka chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au chuo kingine chochote kinachotambulika na Serikali.

ii. Mshahara.

Atalipwa Mshahara wa TGS B sawa na Tshs. 390,000/= kwa mujibu wa Waraka wa Mshahara Serikalini wa mwaka 2015/2016.

iii. Majukumu ya Mtendaji Kijiji

- i. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji;
- ii. Kusimamia ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji,
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Jamii.
- iv. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- v. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu;


- vi. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalisha mali;
- vii. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya kitaalam katika kijiji
- viii. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji.
- ix. Mwenyekiti wa Kikao cha Wataalamu waliopo katika kijiji
- x. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi.
- xi. Kusimamia utungaji wa sheria ndogo za kijiji na
- xii. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

MASHARTI YA JUMLA YA MUOMBAJI KAZI

- Awe Raia wa Tanzania.
- Awe hajawahi kufungwa wala kupatikana na hatia katika makosa yoyote ya jinai.
- Awe na miaka 18-45.
- Mwombaji mwenye cheti cha kughushi asijaribu kuomba nafasi hizi, endapo atabainika hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.
- Awe hajawahi kufukuzwa kazi, kupunguzwa, kuachishwa au kustaafishwa kazi katika Utumishi wa Umma.
- Awe tayari kufanya kazi kijiji chochote ndani ya Wilaya ya Kishapu.
- Waombaji waambatishe vivuli vya vyeti vya Shule, Taaluma, Kuzaliwa na vitambulisho vya Taifa kwa wale walioandikishwa.
- Curriculum Vitae (CV) – Taarifa binafsi ya mwombaji
- Kila mwombaji aambatishe na picha ndogo 1 passport size zilizopigwa hivi karibuni.
- Kila mwombaji aandike kwa usahihi anwani yake na namba ya simu inayopatikana muda wote kwa ajili ya mawasiliano.
- Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **30/11/2020 saa 9:30 Alasiri.**
- Maombi yote yaandikwe kwa mkono bila kuchapwa.
- Maombi yote yawasilishwe kwa anwani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji (W)
S.L.P 1288
KISHAPU

NB: Masharti yaliyoainishwa kwenye Tangazo hili yasomwe kwa makini na yazingatiwe.



Emmanuel Johnson
Mkurugenzi Mtendaji (W)
KISHAPU

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
KISHAPU**

Nakala

- Katibu Tawala (M)
- Halmashauri zote za Mkoa wa Shinyanga
- Mbao za Matangazo
- Waheshimiwa Madiwani wote
- Watendaji wa Kata wote
- Soma website ya Halmashauri.